



## Changamoto na suluhu za usimilishaji wa vielelezo katika fasihi ya watoto: mfano kutoka wasifu wa Mwana Kupona wa King'ei (2008)

Stephen Mwendwa\*, Pamela Ngugi, Catherine Ndungo

Idara ya Kiswahili, Shule ya Sheria, Sanaa na Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya

### IKISIRI

### KUHUSU MAKALA

Makala hii imechunguza changamoto na suluhu zinazotokana na vielelezo vilivyosimilishwa katika Wasifu wa Mwana Kupona (King'ei, 2008). Tafiti kuhusiana na usimilisho wa vielelezo zimefanywa katika hadithi za watoto za Kiswahili. Kwa mfano, Mwendwa (2020) na Mwendwa na wenzake (2021) walichanganua usimilisho wa vielelezo na aina za vielelezo viliyotumika katika hadithi za watoto. Ni dhahiri kwamba, nyingi ya tafiti hizi za awali hazijahusisha moja kwa moja hadithi ya Wasifu wa Mwana Kupona (2008) na changamoto zinazoibuka katika harakati ya kusilimilisha vielelezo. Ni muhimu kuonyesha kuwa katika harakati ya usimilishwaji, changamoto fulani hutokea. Ni katika msingi huu ndipo makala hii imeshughulikia changamoto na suluhu za usimilishwaji wa vielelezo katika Wasifu wa Mwana Kupona. Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Usimilisho ya Bluestone (1957) iliyoendelezwa na Goodman (1976), Andrew (1984) na Starrs (2006). Nadharia ya Usimilisho inahusu uzalishaji wa kazi nyingine huru baada ya kazi ya awali kuzalisha kazi nyingine. Data iliyotumika katika makala hii imetolewa maktabani. Mathalan, majarida, tasnifu, na vitabu vinavyohusiana na makala hii yalisomwa. Vilevile, usomaji, uchambuzi na hata unakili wa vipengele muhimu vinavyohusiana na hadithi teule ulifanywa. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa, changamoto za vielelezo vilivyosimilishwa vinaweza kutokana na mchoraji wa vielelezo vya fasihi ya watoto, uwiano wa picha na matini, usawiri wa wahusika kupitia vielelezo, mandhari katika hadithi na matumizi ya rangi. Aidha, imebainika kuwa vielelezo vinaweza kutumika kupasha ujumbe iwapo vitatumika kwa njia faafu.

#### Maneno Muhimu:

Fasihi ya Watoto,  
Usimilishaji,  
Vielelezo

#### Historia ya Makala:

Tarehe ya Kutumwa: 18 Juni 2024  
Tarehe ya Kurekebisha: 30 Julai 2024  
Tarehe ya Kukubalika: 10 Septemba 2024  
Mtandaoni: 27 Novemba 2024

### 1. Utangulizi

Makala hii ina sehemu zifuatazo; utangulizi, muhtasari wa Wasifu wa Mwana Kupona, dhana ya Fasihi ya Watoto, msingi wa Nadharia, mbinu za Utafiti, changamoto na suluhu za usimilishwaji wa vielelezo katika Wasifu wa Mwana Kupona na hitimisho.

Dhana ya usimilisho imeelezwa na wataalamu tofauti kwa mfano, Muthubi (2005) anasema kwamba, usimilishwaji ni ile hali ya kuifanyia matini chasili marekebisho yanayofaa ili uweze kuibuka na matini lengwa ambayo itafaa hadhira ya watoto ambao ni walengwa tofauti na waliolengwa na matini chasili. Vilevile, Kauli (2011) anaeleza usimilisho kama hali ya kuipa matini inayopatikana katika utanzu fulani wa fasihi sifa za matini nyingine katika utanzu tofauti wa fasihi. Kwa mfano, utanzu wa ushairi unaweza kubadilishwa na kuwa hadithi ya watoto kama vile; Utenzi wa Mwana Kupona (1972) ulisimilishwa na kuwa Wasifu wa Mwana

Kupona (WMK) (King'ei, 2008). Kwa mujibu wa Omuya (2017) usimilishwaji ni hali ya kurekebisha au kubadilisha, kuunda upya baadhi ya vipengele katika matini chasili kama vile ploti, majina ya wahusika, mtindo wa lugha na maudhui ili kulenga hadhira tofauti na ile iliyolengwa na matini chasili. Kwa hivyo, similisho ni hali ya kuipa matini, inayopatikana katika utanzu fulani wa fasihi, sifa za matini nyingine katika utanzu tofauti wa fasihi kwa lengo la kusomwa na hadhira tofauti na ile iliyokuwa mwanzoni. Lengo la makala hii ni kuchunguza changamoto zinazotokana na usimilisho wa vielelezo katika WWM (King'ei, 2008) na kuzitolea suluhu.

Usimilishwaji wa vielelezo katika fasihi ya watoto ni muhimu kwa sababu, huwasaidia watoto kuelewa kazi ambazo zimeandikwa au hata kusimilishwa (Schallert, 1980). Kauli hii imeungwa mkono na Wiesner (1991) ambaye anaongeza kuwa, vielelezo husaidia kukuza

\* Mwandishi Mkuu. Simu: +254720718608; Barua Pepe: [mwendwastins@yahoo.com](mailto:mwendwastins@yahoo.com)

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kenya

Nukuu: Stephen M., Pamela N., & Catherine N. (2024). Changamoto na Suluhu za Usimilishaji wa Vielelezo katika Fasihi ya Watoto: Mfano kutoka Wasifu wa Mwana Kupona wa King'ei (2008). Jarida la Kiswahili Sanifu 1 (2024), 8 – 17.

ubunifu wa watoto. Amedhihirisha hili katika kitabu chake kiitwacho Tuesday ambapo ametumia vielelezo pekee yake bila ya kuviambatanisha na maandishi. Katika kufanya hivi, analenga kuwafikirisha watoto wanaozitazama picha hizo waweze kutabiri yatakayotokea katika hadithi hiyo na hivyo kuwafanya wabunifu zaidi. Nodelman (1996) anashadidia kauli hii kwa kusema kuwa, watoto huhitaji picha katika kazi zao kwa sababu wao huelewa vielelezo kwa haraka ikilinganishwa na maandishi. Isitoshe, watoto huelewa maandishi zaidi iwapo yataambatanishwa na vielelezo. Katika harakati ya kusilimisha vielelezo, changamoto hutokea kwa mfano; changamoto zinazotokana na mchoraji wa vielelezo vya Fasihi ya Watoto, changamoto zinazotokana na uwiano wa picha na matini, changamoto za usawiri wa wahusika kupitia vielelezo, changamoto zinazokumba mandhari katika hadithi na changamoto zinazotokana na matumizi ya rangi.

### 1.1. Muhtasari wa Wasifu wa Mwana Kupona

Utenzi wa Mwana Kupona umesilimishwa mara mbili na Kitula King'ei. King'ei aliusilimilisha Utenzi wa Mwana Kupona kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 2000 katika Kiingereza na kuuita Mwana Kupona: Poetess from Lamu (MKPL) (King'ei, 2000). Mnamo mwaka wa 2008 aliusilimisha tena utenzi uo huo katika Kiswahili na kuuita WMK (King'ei, 2008).

Hadithi ya MKPL (King'ei, 2000) ni kisa cha kusisimua ambacho kimeelezwa kupitia dayolojia, vichekesho na hata mtiririko wa vitushi vya hadithi. Hadithi ya MKPL (King'ei, 2000) imejengwa na maudhui ya mapenzi, maisha, dini ya Kiislamu na hata sehemu za shairi kutoka Utenzi wa Mwana Kupona (Sheikh & Nabhany, 1972). Aidha, hadithi hii imeshugulikwa utunzi wa ushairi wa Kiswahili na hata maisha ya Lamu. Mathalan, vielelezo vimetumika katika baadhi ya kurasa labda kwa lengo la kuisitiza yale yalioandikwa kwenye matini. Hadithi ya MKPL (King'ei, 2000) ni faafu kwa watoto na hata watu wazima. Similisho la pili la WMK (King'ei, 2008) sawia na MKPL (King'ei, 2000) limejengwa kwa vielelezo vilivyotiwa rangi na maandishi katika matini. Hadithi ya Wasifu wa Mwana Kupona (King'ei, 2008) imejengwa na maudhui ya ndoa, nafasi ya mwanamke, mapenzi, dini ya Kiislamu, urafiki miongoni mwa maudhui mengine. Maudhui haya yamejengwa kupitia wahusika kama vile; Mwana Kupona, Zuhura, Mwana Hashima, Abu, Mohammed miongoni mwa wahusika wengine. Mwisho, ni wazi kwamba, masimilisho yote mawili yaani; MKPL (King'ei, 2000) na WMK (King'ei, 2008) yalimlenga mtoto tofauti na Utenzi wa Mwana Kupona (1972) ambao ulimlenga mwanamke aliyekuwa tayari kwa ndoa.

### 1.2. Dhana ya Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ni ile ambayo msingi wa kidhamira na kimaudhui huwarejelea watoto. Fasihi ya watoto ni mpya ikilinganishwa na ile ya watu wazima kwa sababu imeanza kuangaliwa kwa upekee wake hasa kuanzia karne ya 18 (Wamitila, 2008). Watoto huwa na hadithi zao ambazo zinawalenga. Hadithi za watoto huwa na lugha nyepesi, mwega wake wa kidhamira ni watoto wenyewe na huwa zimesheheni vielelezo. Mara nyingi, kazi za fasihi zinazowalenga watoto lazima ziwe na

vielelezo. Vielelezo hivi huweza kuwa michoro au picha. Hii hufanya mtoto avutiwe zaidi na kuwa makini na ile kazi ya fasihi na kuona uhalisia wa kile anachokisoma. Pia, humfanya mwandishi kujiaminisha na kile anachowakilisha kwa hadhira yake ya watoto (Bakize, 2014). Vielelezo ni picha au umbo la kitu au mtu lililoandikwa, kuchorwa au kupigwa chapa au taswira ya mtu au kitu kinachopatikana kutokana na kuvutwa kwa kivuli cha kitu hicho kwa kutumia kamera (TUKI, 2006). Hii ina maana kwamba, kitu hiki kinaweza kuwasilisha kielelezo cha mtu, gari, nyumba na mandhari mbalimbali ili kufanikisha mawasiliano.

Kwa mujibu wa Hunt (2006), vielelezo ni vipengele ambavyo hutumika kuwasilisha ujumbe changamano hasa kwa kusawiri vitu halisi kutoka kwa jamii au ulimwengu halisi. Aidha, Hunt (2006) anaongeza kwamba, vielelezo ni vipengele muhimu vya kuwasilisha ujumbe tofauti na njia ya maandishi katika matini ambayo imezoeleka na wengi. Kiefer na wenzake (2007) wanasema kwamba, vielelezo ni vifaa vya kimsingi vinavyotumika kufunzia watoto katika fasihi ya watoto. Kwa mujibu wa Sohaimi (2011) vielelezo ni michoro ya kila aina inayotumika ndani na nje ya kitabu ili kurembesha umbo na mtindo wa kitabu. Kulingana na Sever (2012), vielelezo ni ujumi unaochochea uundaji wa ujumbe na unafafanua maana ya maandishi yaliyoko kwenye matini kwa kina. Omuya (2017) anaeleza kwamba, vielelezo ni picha au mchoro unaotumiwa kuonyesha au kuelezea kitu halisi katika fasihi ya watoto. Picha hizo huwa zimechorwa au kupigwa chapa. Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, ni dhahiri kwamba vielelezo ni vipengele ambavyo hutumika kupasha ujumbe katika matini. Vielelezo na maandishi huingiliana kwa kuwa, huwa na lengo la kupitisha ujumbe sawia.

### 1.3. Msingi wa Nadharia

Makala hii ilijikita kwenye Nadharia ya Usilimisho iliyoasisiswa na Bluestone (1957). Mwasisi Bluestone, anasema kwamba, usimilisho wa kazi moja hadi nyingine huzalisha kazi nyingine huru inayojitawala. Kulingana na mawazo yake, haiwezekani kazi inayosimilishwa ikailanda similisho lake, kwani wasimilishaji huongeza, huondoa na pia kubatilisha vijisehemu vya kazi asilia. Maoni ya Bluestone (1957) yaliendelezwa na waitifaki kama vile; Goodman (1976), Andrew (1984) na Starrs (2006). Waitifaki hawa wanakubaliana kwamba, ni vigumu kuibuka na similisho sahihi ama aminifu kwa matini chasili kwa sababu ya tofauti za kitamaduni, kimazingira na hata kimtindo.

Kulingana na Nadharia ya Usimilisho, msimilishaji hutakiwa kuhamisha vipengele vya maana ya matini chasili kwa matini lengwa kama vinavyobainishwa na mwandishi wake. Kwa hivyo, hana budi kuzingatia mtazamo wa mtunzi kuhusu wahusika na uhusika wao, maudhui, hali ya usimuliaji, mandhari, mbinu na kadhalika ili vipengele hivi viwasilishe maana kama alivyokusudia mwandishi. Mhimili huu ni faafu kwa vile umewaoongoza watafiti kuchanganua changamoto na suluhu za matumizi ya vielelezo zinazojitokeza katika hadithi teule.

## 2. Mbinu za Utafiti

Kusoma na kuchanganua WMK (King'ei, 2008) ndizo mbinu kuu ambazo zimetumika kukusanya data. Watafiti wamesoma, wamenakili na hata kuchambua masuala muhimu kuhusu changamoto na suluhu zinazokumba vielelezo haswa katika hadithi za watoto. Ili kufanikisha lengo hili, watafiti wametumia mbinu ya uchunzaji kuchambua vielelezo katika similisho teule. Kulingana na Kothari (2009), uchunzaji ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kutazama matukio mbalimbali katika mazingira halisi ya utokeaji. Vilevile, watafiti wameiteua hadithi ya WMK (King'ei, 2008) kimaksudi. Uteuzi wa kimaksudi wa data unahusu uteuzi wa moja kwa moja wa data yenye sifa zinazolengwa na utafiti husika (Komb & Tromp, 2006). Hivyo basi, matini teule ilichaguliwa kimaksudi. Watafiti wamepitia kwa kina hadithi teule ili kuainisha changamoto zinazoambatana na vielelezo katika kazi za watoto.

## 3. Matokeo na Majadiliano

### 3.1. Changamoto na Suluhu za Usimilishwaji wa Vielelezo katika Wasifu wa Mwana Kupona

Katika similisho la WMK (King'ei, 2008), changamoto zinazokumba vielelezo zimeelezwa. Aidha, changamoto hizo zimetolewa suluhu. Matini asilia iliyotumiwa kusimilisha hadithi ya WMK (King'ei, 2008) ni Utenzi wa Mwana Kupona (Sheikh & Nabhany, 1972). Mchoraji wa vielelezo katika similisho la WMK (King'ei, 2008) ni George Obonyo. Changamoto hizo ni kama vile mchoraji wa vielelezo, uwiano wa picha na matini, usawiri wa wahusika kupitia vielelezo, kipengele cha mandhari na matumizi ya rangi.

### 3.2. Changamoto zinazotokana na Mchoraji wa Vielelezo vya Fasihi ya Watoto

Kulingana na Best Accredited College (2022), waandishi na wachoraji ni wasanii wabunifu ambao hutumia vipawa vyao vya utunzi wa hadithi kwa njia ya kiusanii ili kuwafikia walengwa wao. Waandishi hutumia maandishi kutamba hadithi ilhali wachoraji hutumia vielelezo kupitisha ujumbe wa hadithi. Waandishi na wachoraji hushirikiana kwa pamoja ili kufakinisha kazi ya utunzi. Waandishi hutumia muda wao kutunga hadithi kupitia maandishi huku wachoraji wakiitafsiri matini iliyotungwa kupitia vielelezo ili kuwasilisha ujumbe ule mwandishi alikusudia. Kwa mujibu wa Ruthiri (2012), katika matumizi ya vielelezo, mwandishi na mchoraji wa vielelezo wanahitaji kuhakikisha kuwa vielelezo vimewasilishwa kwa namna ambayo watoto wanaweza kuelewa kwa haraka. Vilevile, wahakikishe kuwa vielelezo hivyo vinaakisi vitendo vya wahusika na vinaoana na ujumbe uliokusudiwa. Kulingana na Mello (2016), wachoraji wanastahili kutilia maanani suala la hadhira lengwa ambao ni watoto. Mello (Keshatajwa) anaongeza kwamba, iwapo kitabu kitalenga watoto ambao wanaweza kusoma, vielelezo vitumike ili kueleza hadithi kwa njia rahisi. Vielelezo hivi vitatumika kuchanganua hoja muhimu katika ploti ya hadithi husika.

Vielelezo vinastahili kueleweka kwa urahisi na visichukue ukurasa mzima katika matini kwani ujumbe huenda ukaathiriwa na hivyo basi kupoteza maana

iliyokusudiwa na mwandishi. Matumizi ya vielelezo katika hadithi ya WMK (King'ei, 2008) ni faafu kwani mchoraji hajatumia ukurasa mzima kuweka kielelezo. Hata hivyo, kuna baadhi ya changamoto zinazoambatana na vielelezo katika hadithi teule. Kwa mfano, tazama kielelezo cha 1 katika WMK (King'ei, 2008: 12) kama ilivyojadiliwa katika Tak. 1.



Tak. 1: Mfano wa kielelezo cha 1 kutoka WMK (King'ei, 2008: 12)

Bluestone (1957), Goodman (1976), Andrew (1984) na Starrs (2006) wanakubaliana kuwa, msimilishaji hutakiwa kuhamisha vipengele vya maana ya matini chasili kwa matini lengwa kama vinavyobainishwa na mwandishi wake. Kwa hivyo, hana budi kuzingatia mtazamo wa mtunzi kuhusu wahusika na uhusika wao ili kipengele hiki kiwakilishe maana kama alivyokusudia mwandishi. Aidha, kielelezo hiki cha 1 kutoka WMK (King'ei, 2008: 12) kimezua changamoto. Kwa mfano, si rahisi kuwatambua wahusika waliosawiriwa katika kielelezo hiki.



Tak. 2: Mfano wa kielelezo cha 2 kutoka WMK (King'ei, 2008: 23)

Huenda wahusika wale ni Mwana Hashima na Zuhura, lakini changamoto ni kuwa, wahusika hawa wanabadilikabadilika kutoka kielelezo kimoja hadi kingine. Mello (2016) anasisitiza kwamba, vielelezo vya watoto vinastahili kuwa na mfuatano wa kuaminika hivi kwamba, wahusika wanaosawiriwa kutoka mwanzo wa hadithi wanabaki kuwa wale wale; yaani;

wasibadilikebadilike kutoka ukurasa mmoja hadi ukurasa mwingine. Kauli ya Mello (2016) haijazingatiwa katika uchapishaji wa vielelezo katika kielelezo cha 1 katika WMK (King'ei, 2008: 12) kwani sura za wahusika zinabadilikabadilika kutoka kielelezo kimoja hadi kingine.



Tak. 3: Mfano wa kielelezo cha 3 kutoka WMK (King'ei, 2008: 27)

Kulingana na Waffles (2014) mchoraji wa vielelezo anastahili kumchora mhusika wake mara kadha wa kadha ili kuhakikisha kwamba, mhusika yule anabakia vile licha ya kuchorwa katika mandhari tofauti tofauti katika hadithi. Vilevile, mchoraji anastahili kuchora maumbo ya vielelezo ambayo si tata kwani kwa kufanya hivyo, huenda wahusika wake wasibadilikebadilike kutoka kielelezo kimoja hadi kingine. Muhimu zaidi ni kuwa mwandishi na mchoraji wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili mwandishi athibitise kuwa vielelezo vya mchoraji vinaafikiana na hadithi yake.



Tak. 4: Mfano wa kielelezo cha 4 kutoka WMK (King'ei, 2008: 62)

Katika Tak. 4 katika WMK (King'ei, 2008:12) msomaji anaweza kukisia kwamba, wahusika wale ni Mwana Hashima na Zuhura. Ili kuondoa utata huo wa kubadilikabadilika kwa wahusika, ni vyema wachoraji wazingatie utaratibu wa kuaminika hasa kwa vielelezo vyote vilivyo ndani ya matini. Wachoraji wawachore wahusika bila ya kubadilisha nyuso wala maumbo yao ili kuzuia kuwakanganya watoto kwani kwa kufanya hivyo, wataondoa dhana ya kukisia.

Mifano mingine ni katika Tak. 2 na Tak. 3 ambapo sura za Mwana Hashima na Zuhura zinabadilika. Aidha,

sura ya Mwana Hashima katika kielelezo cha 4 ni tofauti kabisa na vielelezo vingine ambavyo amesawiriwa. Isitoshе, mchoraji wa vielelezo katika similisho la MKPL (King'ei, 2000) anaweza kutumia suluhu iliyopendekezwa kwa similisho la WMK (King'ei, 2008). Hii ni kwa sababu, katika matini zote mbili kuna kubadilikabadilika kwa sura za wahusika.

### 3.3. Changamoto zinazotokana na Uwiano wa Picha na Matini

Tanaka (1994) anasema kwamba, picha huchukuliwa kama kitengo kimojawapo cha usemi, kinachotarajiwa kuwasiliana na wapokezi kwa kuchochea au kusaili dhana fulani. Picha huwa na sura na sifa za usemi zinazojidhihirisha katika msuko. Msuko wa picha huwa na mchango mkubwa katika kuathiri mkondo wa maana na ujumbe kwa wapokezi. Kulingana na Knowles na Malmkjaer (2002), vielelezo ni muhimu sana kwani humsaidia msomaji kuelewa mwingiliano uliopo baina ya hadithi, lugha na ulimwengu jambo ambalo huipa hadithi uhai. Wanaongeza kwamba, vielelezo humpa mtoto nafasi ya kuwa na mwingiliano wa moja kwa moja na matini kwa sababu vinasimua hisia zake na pia kumfundisha jinsi ya kuyatumia maneno kuashiria kitu fulani.



Tak. 5: Mfano wa kielelezo cha 5 kutoka WMK (King'ei, 2008: 70)

Uwiano wa picha na matini katika fasihi ya watoto ni jambo la kutiliwa maanani kwa sababu mtoto anapoisoma ile matini na kisha kutazama kile kielelezo kilichowekwa pale, anastahili kuona mwingiliano wa picha na matini ili kuzuia mtiririko wa vitushi ambavyo vinaingiliana. Iwapo picha na matini zinaingiliana basi hadithi itaeleweka kwa urahisi na si vinginevyo.

Katika hadithi ya WMK (King'ei, 2008) mchoraji wa vielelezo hajatilia mkazo suala hilo la uwiano wa picha na matini na hivyo basi, kusababisha utata hasa katika baadhi ya vielelezo. Hata hivyo, suluhu imependekzwa katika changamoto hiyo ya uwiano wa picha na matini. Tazama mfano wa King'ei, (2008) katika kielelezo cha Tak. 5 kimesawiri minazi, bahari na nyumba za kifahari. Angani kuna ndege ambao wanaruka juu. Kielelezo hiki cha Tak. 5 (King'ei, 2008:70) kimezua utata kutokana na jinsi kilivyosawiriwa na hasa ule uwiano wake na matini katika hadithi ya WMK (King'ei, 2008).

Katika Tak. 5 huenda mchoraji amesawiri eneo ambalo familia ya Mwana Kupona ilikuwa inaelekea. Hata

hivyo, kielelezo hiki kimezua maswali mengi kutokana na mahali ambapo kimewekwa na hasa mwingiliano wake na matini. Kielelezo hiki cha WMK 5 (King'ei, 2008:70) hakiambatani na mtiririko wa hadithi katika matini. Hii ni kwa sababu, katika matini, mwandishi anazungumzia kuhusu mhusika mzee Abu ambaye alikuwa anamwonyesha Mwana Hashima merikebu kubwa ambayo ilikuwa ikielekea upande wao huku ikiwa imebeba shehena ya mikoko kupeleka Uarabuni. Kielelezo hiki cha Tak. 5 kinakinzana na yale yanayoelezwa katika hadithi na hivyo basi, hakifai katika sehemu kilichopachikwa katika similisho la WMK (King'ei, 2008). Kielelezo hiki kina vuruga mtiririko wa vitushi katika hadithi.

Kwa mujibu wa Elster na Simons (1985) uwiano wa picha na matini huathiri upokezi wa uelewa wa hadithi. Mtoto anapoisoma matini na kisha kutazama kielelezo kilichowekwa pale, anastahili kuona mwingiliano wa picha na matini ili kuzua mtiririko wa vitushi ambavyo vinaingiliana. Ni wazi kwamba, katika kielelezo hiki cha WMK 5 (King'ei, 2008:70) hakiambatani na yale yanayojadiliwa katika hadithi kwani, kimesawiri mandhari tofauti na yale yanayozungumziwa katika hadithi. Hivyo basi, kielelezo hiki hakifai katika sehemu kilichopachikwa kwani hakiambatani na mtiririko wa vitushi vya hadithi.

Kutokana na changamoto hii katika hadithi teule ya WMK (King'ei, 2008), suluhu imependekezwa kwa kipengele hiki cha uwiano wa picha na matini. Rejelea mfano wa WMK 5 (King'ei, 2008: 70). Kwanza, kungekuwepo na mwingiliano wa picha na matini iwapo mchoraji angechora kielelezo kinachosawiri wahusika; mzee Abu, Mwana Hashima na hata shehena ambalo linabeba mikoko kwa sababu hayo ndiyo masuala yaliyopo kwenye matini. Kwa kufanya hivyo, huenda uwiano wa picha na matini ungeeleweka bila utata na hivyo basi, kumfanya mtoto kuelewa yanayojadiliwa kwa matini kupitia kwa kielelezo.

### 3.4. Changamoto za Usawiri wa Wahusika Kupitia Vielelezo

Kulingana na Mbatiah (2001), wahusika ni watu tunaokutana nao katika kazi ya kifasihi na ambao kutokana na matendo na mazungumzo yao wanatadokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika. Aidha, Tylor (2017) anasema kwamba, japo kila kipengele cha sanaa huwa na upekee fulani, vielelezo huonekana kama kipengele muhimu cha kupitisha ujumbe. Mathalan, vielelezo hutumika kupitisha ujumbe fulani kama vile maneno katika matini. Isitoshe, maneno hutumika kufasiri vielelezo. Hivyo, maneno na vielelezo ni vipengele ambavyo hutegemeana sana.

Wahusika wanaweza kuwasilishwa kupitia vielelezo au maandishi. Katika hadithi ya WMK (King'ei, 2008) matumizi ya wahusika yapo. Baadhi ya wahusika hawa ni wanyama na binadamu. Kwa mfano, kuna wahusika binadamu kama vile; Mwana Kupona, Mwana Hashima, Zuhura, Mohammed, Fatuma, Kombo, Abu, Mtume Mohammed miongoni mwa wahusika wengine. Kwa upande wa wahusika wanyama kuna; ngamia, paa na wanawe.

Usawiri wa wahusika katika kazi ya fasihi ya watoto na haswa vielelezo vinavyowahusisha wahusika ni suala ambalo linahitaji kuchukuliwa kwa uzito wake na wachoraji. Kwa kufanya hivyo, huenda wachoraji wakazuia maswali mengi miongoni mwa watoto ambao kwa mara nyingi huwa wadadisi na pia wahakiki wa kazi zao. Iwapo mchoraji hatakamilisha mchoro wake ipasavyo, basi huenda watoto wakawa na maswali mengi kuhusiana na mchoro ule kama vile; kukosa kuweka mhusika miguu, kutotumia rangi inayofaa na kutoweka uhalisia ndani ya picha miongoni mwa mambo mengine. Kuna baadhi ya vielelezo ambavyo huenda vitazua maswali baina ya watoto katika WMK (King'ei, 2008). Hata hivyo, utafiti ulihusisha kielelezo kimoja kama mfano. Tazama kielelezo cha Tak. 6 (King'ei, 2008). Aidha, changamoto zinazotokana na kielelezo hiki zimependekezwa suluhu.



Tak. 6: Mfano wa kielelezo cha 6 kutoka WMK (King'ei, 2008: 23)

Katika kielelezo cha Tak. 6 kuna wahusika watatu ndani ya chumba ilhali nje kuna umati wa watu waliosimama huko katika makundi labda katika shughuli zao za kibiashara au hata maongezi. Katika kielelezo hiki cha Tak. 6, kuna wanawake wawili waliosimama huku wakiwa wameshika khanga ambayo imechorwa kielelezo kinachoashiria mapenzi. Khanga hiyo pia, imeandikwa mapenzi ni kikohozi. Kielelezo hiki kimetumika kuwasilisha maudhui ya mapenzi na urafiki haswa baina ya Mwana Hashima na Zuhura ambao ni marafiki. Marafiki hawa wawili wamevalia buibui na kujifunika hijabu kichwani kama njia ya kufuata mila na desturi za Waswahili na haswa wanawake kutoka dini ya Kiislamu. Mwana Hashima na Zuhura walikuwa kwenye duka kununua vitu walivyokuwa wakivihitaji katika harusi ya Zuhura.

Mchoro huu wa Tak. 6 huenda ukazua changamoto kutokana na vile ulivyosawiriwa na mchoraji. Kwanza, Mwana Hashima na Zuhura wamechorwa bila miguu na hivyo basi kuzua maswali kwa mtoto anayeisoma kazi ile iwapo wahusika wale walikuwa walemavu au la. Mathalan, ndani ya chumba kile, kuna mwanaume ambaye amevalia kofia na huenda ndiye muuzaji pale. Mhusika yule hana macho wala uso na hivyo basi, kukifanya kielelezo hiki cha WMK 6 (King'ei, 2008:23)

kuwa tata. Huenda basi, kielelezo hiki kikakosa kutimiza lengo la mwandishi.

Isitoshe, kwenye matini, mwandishi anaeleza kwamba Mwana Hashima na Zuhura waliingia ndani ya maduka mawili ilhali kielelezo cha [Tak. 6 \(King'ei, 2008:23\)](#) hakijasawiri duka inavyostahili. Hii ni kwa kuwa, mchoro ule unafanana na kibanda bali si duka. Wakati mwingine, watoto hutumia vielelezo ili kuelewa matini kwa kina na hii ni kutokana na msamiati mpya ambao mwandishi ametumia katika matini ([Calabrese, 2010](#)). Hivyo basi, kutovichora vielelezo kwa njia inayostahili huenda kukazua changamoto miongoni mwa watoto ambao hutazama vielelezo ili kupata maana zaidi ya yale yalioandikwa kwenye matini. Vilevile, ni dhihirisho kuwa kazi za watoto hazichukuliwi kwa dhati na wanajamii wengi ambao huwa wanazipuuza.

Pia, katika matini, mwandishi anasema kwamba khanga walioshika Mwana Hashima na Zuhura ilikuwa ni ya rangi ya samawati ilhali kwa kutazama kielelezo hiki cha [Tak. 6](#) ni wazi kwamba rangi alioitaja mwandishi haiwiani na ile iliyotumiwa kwenye khanga. Khanga hii ina mseto wa rangi mbalimbali kama vile rangi nyeusi, nyeupe na hata waridi. Rangi iliyotajwa katika matini ambayo ni ya samawati haijatumika mahali popote na hivyo basi, kuzua utata kuhusiana na kielelezo hiki hasa kwa hadhira lengwa. Aidha, mchoraji amewacha nafasi ya kukisia kuhusiana na kielelezo hiki cha [Tak. 6](#) na hii ni kutokana na usawiri mbaya wa majora yaliyoko juu ya meza. Majora yaliyochorwa katika mfano wa WMK 3 ([King'ei, 2008:23](#)) huenda yakatatiza kwani si kamilifu na hayajatumikiza matumizi ya rangi ipasavyo.

Mathalan, kuna umati wa watu ambao unaoonekana nje ya mlango. Hata hivyo, umati huu hauna mchango kwa matukio katika hadithi. Ni wazi kwamba, mchoro huu umezua baadhi ya maswali na hivyo huenda ukasababisha changamoto kwa mtoto ambaye ndiye hadhira lengwa na hii ni kutokana na vile mchoraji alivyowasawiri wahusika wake katika kielelezo hiki cha [Tak. 6](#).

[Bakize \(2014\)](#) anasema kuwa, fasihi ya watoto huzingatia uhusika wa watoto wenyewe. Hata hivyo, anaongeza kwamba, hata kama kutakuwa na wahusika ambao ni watu wazima, lazima wahusika wakuu au waathirika wa kazi ya fasihi wawe watoto. Mfano huu wa [Tak. 6](#) hauingiliani na maoni ya [Bakize \(2014\)](#) kwa sababu, ukitazama kielelezo hiki cha WMK 6 (2008: 23) wahusika wakuu ambao ni Zuhura na Mwana Hashima huenda wakamtatiza mtoto kwani nyuso zao zinawiana na zile za wanawake ambao wamevunja ungo na wako tayari kwa ndoa.

Katika mchoro huu wa [Tak. 6](#) kuna baadhi ya mambo ambayo yalistahili kusawiriwa ipasavyo ili kuondoa utata. Kwanza, Mwana Hashima na Zuhura wangechorwa kwa kuwekwa miguu ili wasije wakasawiriwa kama kwamba wao ni walemavu. Mathalan, muuzaji ndani ya duka lile alistahili kuwekwa macho na uso ili kuweka uhalisia katika kielelezo hiki cha [Tak. 6](#). Isitoshe, kwenye matini, mwandishi anaeleza kwamba Mwana Hashima na

Zuhura waliingia ndani ya maduka mawili ilhali kielelezo cha WMK 6 hakijasawiri duka inavyostahili kwa maana mchoro ule unafanana na kibanda bali si duka. Hivyo basi, mchoraji alistahili kuchora duka inavyostahili ili kuondoa mkanganyo.

[Calabrese \(2010\)](#) anasema kwamba, watoto hupenda sana na ndio sababu wasanii wengi haswa wachoraji hutumia muda wao kuchora vielelezo na hata kuvipaka rangi ili kuwavutia wasomaji lengwa ambao ni watoto. Rangi ni muhimu katika fasihi ya watoto na watoto huchagua vitabu vilivyo na rangi angavu vikilinganishwa na vitabu visivyo na rangi angavu. Aidha, watoto hutambua na kuchagua rangi nyekundu kwanza ikifuatwa na rangi ya majano, samawati na kijani kibichi ([Ruthiiri, 2012](#)). Hivyo basi, suala la rangi katika vielelezo katika fasihi ya watoto ni jambo muhimu. Matumizi ya rangi katika similisho la WMK ([King'ei, 2008](#)) limepuuzwa na hivyo huenda vielelezo vile visipitishie ujumbe lengwa kutokana na matumizi mabaya ya rangi. Kwa mfano, kuna utata unaozunguka matumizi ya rangi kwenye khanga walioshika Mwana Hashima na Zuhura. Katika matini, mwandishi anasema kwamba rangi ya samawati ilitumika kusawiri khanga katika kielelezo cha WMK 6 ([King'ei, 2008:23](#)). Ni dhahiri kuwa, rangi alioitaja mwandishi haiwiani na ile iliyotumiwa kwenye khanga na mchoraji. Khanga iliyosawiriwa ina mseto wa rangi mbalimbali. Kutotumia rangi ya samawati kama alivyopendekeza mwandishi huenda kukazua mkanganyo hasa kwa hadhira lengwa. Hivyo, mchoraji alistahili kutumikiza rangi iliotajwa na mwandishi ndani ya matini. Usawiri wa khanga ya rangi ya samawati huenda ukazuia utata katika kielelezo. Kwa kufanya hivyo, huenda kielelezo kikapitisha ujumbe kwa urahisi kwani matini yatakuwa yanawiana na kielelezo.

Kuhusu umati wa watu ambao umesawiriwa nje ya mlango na hauchangii katika matukio ya hadithi, ingekuwa faafu iwapo mchoraji angewasawiri wahusika wale kwa ukamilifu. Hivyo, uhalisia wa kielelezo hiki cha [Tak. 6](#) ungeonekana.

Aidha, wahusika wakuu katika kielelezo hiki cha [Tak. 6](#) wanastahili kuwa na nyuso ambazo ni za vijana au hata watoto ili kujinasibisha na walengwa kama anavyosema [Bakize \(2014\)](#) kuwa, fasihi ya watoto huzingatia uhusika wa vijana wenyewe. Vilevile, uhalisia wa majora yaliyochorwa katika mfano wa [Tak. 6](#) yalistahili kusawiriwa vizuri hasa kwa kuyatia rangi faafu na kuyachora kwa ukamilifu ili kuleta uhalisia. Mathalan, majora yaonekane vizuri ili kuondoa utata wa kukisia kuwa ni majora. Kwa kuyasawiri majora ipasavyo, huenda watoto au vijana lengwa wakafasili lengo la mchoraji na mwandishi bila utata na hivyo, mtiririko wa hadithi kubakia.

Ni wazi kwamba, changamoto zinatokea kupitia usawiri wa wahusika. Changamoto hizi zipo katika similisho la MKPL (2000) na lile la WMK (2008). Hivyo basi, mchoraji wa vielelezo katika MKPL (2000) anaweza kutumia suluhu zilizopendekezwa kwa similisho la WMK (2008) kama kigezo cha kuondoa utata sawia.

### 3.5. Changamoto zinazobainika katika kipengele cha Mandhari

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mandhari hutumiwa kueleza sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili linaweza kutumika kwa mapana kueleza pia mazingira ya kiteknolojia ya tendo fulani. Wamitila (Keshatajwa) anaongeza kuwa, mandhari ina nafasi na umuhimu mkubwa katika hadithi na kwamba ni lazima msomaji ajitahidi kuangalia kama kuna uhusiano kati ya mandhari na vipengele vingine vya kiutunzi kama wahusika, dhamira, maudhui, ujumbe na kadhalika. Kulingana na Muusya (2012), mandhari ni mahali au makazi maalum yaliyojengwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi. Aidha, Janovsky (2018) anasema kuwa, mandhari ni kipengele muhimu kwa sababu huwa na athari kwa ploti na wahusika katika hadithi.

Kazi za watoto huwa na mandhari mbalimbali na iwapo mandhari hayo yatasawiriwa kwa njia tata, basi huenda ule ujumbe alionuia mwandishi, ukapotea. Hivyo basi, ni jambo muhimu kwa mchoraji yeyote yule kuhakikisha kwamba mandhari ambayo amesawiri kupitia michoro yanaeleweka kwa urahisi. Hata hivyo, katika similisho la Wasifu wa Mwana Kupona (2008) matumizi ya mandhari yamekumbwa na baadhi ya changamoto kama vile katika kielelezo cha WMK 7 (2008: 70). Hata hivyo, suluhu imependekezwwa katika kielelezo hiki cha 7. Tazama mfano wa Tak. 7.

Kielelezo hiki cha Tak. 7 kimesawiri minazi, bahari na nyumba. Angani kuna ndege ambao wanaruka juu. Katika kielelezo cha WMK 7 (2008-Uk: 70) mchoraji alikuwa anasawiri eneo ambalo familia ya Mwana Kupona ilikuwa inaelekea. Baada ya safari ya baharini, wahusika katika jamii ya mwandishi walikuwa wametamatisha safari yao na sasa walikuwa wamefika kwenye ufuo wa bahari. Sehemu hii ndio ambayo imesawiriwa na mchoraji wa Wasifu wa Mwana Kupona (2008) kupitia kielelezo cha Tak. 7. Mandhari ambayo yamesawiriwa yanaonyesha bahari, nyumba, minazi, nazi, michanga tifu tifu kwenye ufuo wa bahari na hata ndege wa angani.



Tak. 7: Mfano wa kielelezo cha 7 kutoka WMK (King'ei, 2008: 70)

Kielelezo hiki cha Tak. 7 (King'ei, 2008:70) huenda kikazua changamoto kwani uhalisia wa mandhari ambayo yamesawiriwa na mchoro huu yana utata. Mandhari ambayo yamesawiriwa hapa si halisi bali ni ya kifantasia. Kulingana na Tucker (1984) ni muhimu matendo

yatendeke katika uelewa na tajriba ya mtoto. Aidha, anaongeza kwamba, watoto wa miaka tisa hadi kumi wana tofauti nyingi zinazohusiana na hali zao za kukomaa, zikiwepo pia tajriba zao. Wale wa miaka kumi na mitatu hadi kumi na mitano wanavutiwa na mandhari halisi, kwa sababu wana shauku ya kujua mambo mapya katika hali halisi ya maisha. Mandhari yanatakiwa yawe yale yanayoaminika na kueleweka.

Mandhari ambayo yanajitokeza katika kielelezo hiki ni ya kifantasia na hivyo basi hayaaminiki hasa kwa hadhira lengwa ambayo ni watoto wanaovutiwa na mambo halisi. Bahari na mawingu yaliyoko katika kielelezo hiki yamesawiriwa kwa rangi ya waridi huku majani ya miti yakiwa ya rangi nyeusi na waridi. Isitoshе, ndege waliosawiriwa kwenye mandhari haya hawana uhalisia wowote kwani hawajachorwa kwa umakinifu na hivyo basi huenda mandhari ya kielelezo hiki cha Tak. 7 yakazua utata na kuchochea kutinga lengo kuu la kupitisha habari. Vilevile, uwiano wa kielelezo hiki cha Tak. 7 na matini haupo na hivyo basi, mandhari yaliyosawiriwa hapa hayana mashiko yoyote na kile kinachozungumzwa ndani ya matini. Kwa mfano, katika matini, mhusika Abu anamwonyesha Mwana Hashima meli iliyobeba mikoko kupeleka Uarabuni lakini kwa kutazama kielelezo cha Tak. 7 mandhari yaliyosawiriwa ni tofauti na yale yanayozungumziwa katika matini. Hivyo, mandhari katika kielelezo hiki cha WMK 7 (King'ei, 2008: 70) yana utata.

Ingekuwa bora iwapo mchoraji angetumia rangi ya samawati au nyeupe kuchora mawingu na kisha kutumia kijani kibichi kuchora majani ya miti. Kwa upande wa ndege, angewachora kwa ukamilifu hasa kwa kuwaweka viungo vyote vya mwili. Kwa kuzingatia mambo haya, huenda ule uhalisia wa mandhari ukatokea na hivyo kuchochea kueleweka kwa mandhari kwa urahisi. Mathalan, Ruthiiri (2012) anasema kuwa, mchoraji anayeamua kutumia mandhari ya kidhahania kama vile katika hadithi za kifantasia ni lazima aeleze kwa undani ili kuunda hadithi inayoweza kuaminika na kueleweka kwa watoto lengwa.

Uwiano wa kielelezo hiki cha Tak. 7 (King'ei, 2008: 70) na matini haupo na hivyo basi, mandhari yaliyosawiriwa hapa hayana mashiko yoyote na kile kinachozungumzwa ndani ya matini. Mchoraji angesawiri mhusika Abu akimwonyesha Mwana Hashima meli iliyobeba mikoko kupeleka Uarabuni na hivyo basi kuleta ule uwiano wa picha na matini. Kwa kufanya hivyo, huenda mandhari katika kielelezo hiki cha Tak. 7 (King'ei, 2008: 70) yakaeleweka kwa urahisi. Mandhari katika hadithi ya MKPL (King'ei, 2000) na WMK (King'ei, 2008) yamekumbwa na changamoto sawia. Hivyo, mapendekezo yaliyotolewa kuhusiana na mandhari katika WMK (2008) yanaweza kutumiwa kama kigezo cha kutatua changamoto za mandhari katika MKPL (King'ei, 2000).

### 3.6. Matumizi ya Rangi

Kwa mujibu wa Ruthiiri (2012) rangi ni muhimu katika fasihi ya watoto na watoto huchagua vitabu vilivyo na rangi vikilinganishwa na vitabu visivyo na rangi.

Aidha, [Ndonye \(2017\)](#) anasema kwamba, rangi ni uhalisia wa tamaduni za ulimwengu na ni kigezo muhimu katika kukadiria na kutathmini mitazamo, falsafa na mionoulimwengu ya maisha ya binadamu ya kila siku. Tamaduni za jamii hutawaliwa na matumizi ya rangi anuwai zinazoashiria mambo muhimu kwa jamii husika. Baadhi ya jamii za ulimwengu huitazama rangi kidhahania ilhali jamii zingine husawiri rangi katika misingi ya mahusiano na mambo mseto katika jamii.

[Ndonye \(2017\)](#) anaongeza kwamba, rangi tofauti tofauti huwakilisha masuala mbalimbali katika jamii tofauti ulimwenguni. Shughuli nyingi katika jamii huonishwa na rangi mbalimbali. Kwa mfano; rangi katika kutabiri au kufasiri matukio, rangi katika kuashiria uzazi hususan jinsia ya mtoto aliyezaliwa, rangi katika matambiko ya michakato ya kumvusha mtoto kutoka hatua moja ya makuzi hadi hatua nyingine, sherehe ya harusi, rangi katika michakato ya jinsi tunavyowazika wafu, rangi kama kiashiria cha mahusiano baina ya binadamu na mifugo au mimea na pia, rangi katika sherehe za kuvuna mazao shambani ni miongoni mwa mambo yanayotawaliwa na matumizi ya rangi mbalimbali.



Tak. 8: Mfano wa kielelezo cha 8 kutoka WMK ([King'ei, 2008: 76](#))

Hivyo basi, suala la rangi katika vielelezo na hasa katika fasihi ya watoto ni jambo muhimu. Matumizi ya rangi katika similisho la WMK ([King'ei, 2008](#)) limepuuzwa na hivyo huenda vielelezo vile visipitishie ujumbe lengwa kutokana na matumizi mabaya ya rangi. Isitoshe, suluhu kwa changamoto zinazoambatana na matumizi ya rangi zimetolewa. Kwa mfano, tazama kielelezo cha [Tak. 8 \(King'ei, 2008: 76\)](#). [Calabrese \(2010\)](#) anasema kwamba, watoto huvutiwa na picha zilizo na rangi kadhaa na ndio sababu wasanii wengi hasa wachoraji hutumia muda wao kuchora vielelezo na hata kuvipaka rangi ili kuwavutia wasomaji lengwa ambao ni watoto. Katika kielelezo hiki kuna, bahari na minazi katika sehemu ya nchi kavu. Vilevile, kuna pomboo wawili ambao ni aina ya samaki ambao wanaruka kutoka ndani ya bahari.

Katika kielelezo cha WMK 8 ([King'ei, 2008: 76](#)), mchoraji amechora kielelezo na kisha kukitia rangi ili kumvutia mtoto msomaji. Mchoro huu wa WMK 8 ([King'ei, 2008: 76](#)) huenda ukamchanganya mtoto hasa kutokana na matumizi mabaya ya rangi katika kielelezo hiki cha [Tak. 8](#). Kwa mfano, bahari iliyosawiriwa katika kielelezo hiki imetiwa rangi ya waridi jambo

linalochochea kuwepo kwa mdahalo kuhusu rangi iliyotumiwa kusawiri bahari. Kielelezo hiki kimekosa uhalisia na huenda kikamkanganya mtoto ambaye anafahamu fika kwamba bahari huwa ya rangi ya samawati. Mtoto ambaye ndiye mlengwa katika matini hii, huenda ataelewa kielelezo hiki iwapo atasoma matini ya WMK ([King'ei, 2008](#)). Hivyo, kielelezo hiki cha [Tak. 8](#) hakiwezi kujisimamia na kutoa maana yake bila ya kuambatanishwa na maandishi katika matini.

Hata hivyo, samaki wa pomboo ambao wamesawiriwa katika kielelezo hiki wamefanana na wale halisi na hivyo basi huenda mtoto hatapata ugumu wa kuwatambua wale samaki. Aidha, mtoto atashangaa mbona samaki wale, wanaruka kwenye mandhari yaliyochorwa na kuwekwa rangi ya waridi. Samaki wale wamesawiriwa kana kwamba, wapo kwenye nchi kavu iliyo na kidimbwi cha maji. Aina ya samaki wa pomboo na hasa wa kima kile hawawezi kuishi katika kidimbwi kilichosawiriwa katika kielelezo hiki cha WMK 8 ([King'ei, 2008: 76](#)). Hata ingawaje, kidimbwi hicho ni bahari kwa mujibu wa mchoraji. Hivyo basi, huenda kielelezo hiki [Tak. 8](#) kikamkanganya mtoto ambaye hutazama vielelezo ili kupanua uelewa wa ujumbe ulioko kwenye matini.

Japo mimea iliyochorwa katika kielelezo hiki imesawiriwa kwa mbali, mimea ile imewekwa rangi ya waridi suala ambalo huenda likazua utata kwa mtoto ambaye ndiye mlengwa. Vile vile, mawingu yaliyosawiriwa katika kielelezo hiki cha [Tak. 8](#) yametiwa rangi ya waridi na hilo si jambo la kawaida kuwa na mawingu ya waridi. Matumizi mabaya ya rangi katika kielelezo hiki cha [Tak. 8](#) huenda hayatasaidia mchoraji kupitisha ujumbe wake alionuia kwani ule uhalisia wa vitu vilivyochorwa umepotoshwa na matumizi mabaya ya rangi. Mchoraji wa kielelezo hiki cha [Tak. 8](#) alistahili kutumia rangi ya samati wakati wa kusawiri bahari. Kwa kufanya hivyo, ule uhalisia wa bahari ungeonekana na hivyo, kielelezo kueleweka kwa haraka. Vilevile, utata kuhusu sehemu walioko samaki ungeondolewa.

Mathalan, mimea iliyochorwa katika kielelezo hiki ingesawiriwa kwa kupakwa rangi ya kijani kibichi badala ya waridi. Kwa kufanya hivyo, huenda mtoto hatatatizika kuyatambua mandhari. Isitoshe, mawingu katika kielelezo cha [Tak. 8](#) yangesawiriwa kwa kutumia rangi nyeupe au hata samawati ili kuleta ule uhalisia. Iwapo matumizi ya rangi katika kielelezo hiki cha WMK 8 ([King'ei, 2008: 76](#)) yangezingatiwa, basi huenda yangesaidia mchoraji kupitisha ujumbe wake kwa urahisi kutokana na ule uhalisia wa kielelezo. Suala la matumizi mabaya ya rangi yapo katika hadithi ya MKPL ([King'ei, 2000](#)) na ile ya WMK ([King'ei, 2008](#)). Hata hivyo, changamoto zinazotokana na matumizi mabaya ya rangi zimeshabiana katika masimilisho yote mawili. Hivyo, suluhu zilizopendekezwa katika WMK ([King'ei, 2008](#)) zinaweza kutumiwa kama kigezo katika MKPL ([King'ei, 2000](#)).

#### 4. Hitimisho

Makala hii imebainisha changamoto zinazokumba uwasilishaji wa vielelezo. Vilevile, suluhu zimetolewa katika changamoto hizo. Baadhi ya changamoto hizo



zinasababishwa na; mchoraji wa vielelezo, uwiano wa picha na matini, usawiri wa wahusika kupitia vielelezo, mandhari katika hadithi na matumizi ya rangi. Pia, watafiti wanapendekeza kuwa, chini ya kila kielelezo kunastahili kuwa na maelezo kidogo kukihusu ili kurahisisha uwasilishaji lengwa kutoka kwa kielelezo. Watafiti walibaini kuwa, ni vyema kwa mchoraji kushirikiana na mwandishi ili kupata lengo lake. Aidha, suala la uhariri wa vitabu vya watoto lizingatiwe kwa makini. Baada ya kukamilisha uchoraji wake, mchoraji anastahili kutuma vielelezo vyake kwa mwandishi wa matini na mchapishaji kupitia kwa barua pepe ili apate nafasi ya kuviangalia na iwapo vinaingiliana na matini husika. Wachoraji hutuma vielelezo vyao kwa mwandishi na mchapishaji ili kupata maoni ya ufaafu wa vielelezo kutoka kwa mwandishi.

### Marejeleo

Andrew, D. (1984). *Concepts in Film Theory*. New York: Oxford University Press.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing press.

Best Accredited College (2022). *Difference Between Author & Illustrator*. Retrieved from [https://study.com/articles/difference\\_between\\_auth\\_or\\_illustrator.html](https://study.com/articles/difference_between_auth_or_illustrator.html)

Bluestone, G. (1957). *Novels into Film*. Berkeley: U.

Calabrese, L. (2010). *How Picture Books Play a Role in a Child's Development*. Retrieved from <https://www.thechildrensbookreview.com/weblog/2010/11/howpicture-books-play-a-role-in-a-child%E2%80%99s-development.10/3/2024>.

Elster, C., & Simons, H. D. (1985). "How Important are Illustrations in Children's Readers?". In, *The Reading Teacher*. Pp. 148-152.

Goodman, N. (1976). *Languages of Art*. Indianapolis: Hackett.

Hunt, P. (2006). *Introduction: The Expanding World of Children's Literature Studies*. In *Understanding Children's Literature* (pp. 11-24). Routledge.

Janovsky, A. (2018). *Elements of a Story*. Retrieved <https://study.com/academy/lesson/setting-in-literature-definition-importance-examples.html>. 01/02/2024

Kau, T. M. (2011). *Tathmini ya Usimilisho wa Riwaya na Hadithi Fupi kwa Wanafunzi wa Sekondari Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kiefer, B. Z., Hepler, S., & Hickman, J. (2007). *Charlotte Huck's Children's Literature*. U.S: The McGraw-Hill Companies.

King'ei, K. (2000). *Mwana Kupona: Poetess from Lamu*. Nairobi: Sasa Sema Publishers limited.

King'ei, K. (2008). *Wasifu wa Mwana Kupona*. Nairobi: Sasa Sema Publishers Limited.

Knowles, M. na Malmakjaer, K. (2002). *Language Control in Children's Literature*. London: Routledge.

Komb, D. K. and Tromp, L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology. Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Limited Publishers.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mello, J. (2016). *How to Illustrate a Children's Book*. Retrieved from <https://feltmagnet.com/drawing/How-to-Illustrate-a-Childrens-Book>. 10/3/2024.

Muusya, J. K. (2012). *Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishaji wa diwani za Pendo la Heba na hadithi nyingine na Mizungu ya Manabii na hadithi nyingine*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Muthubi, F. (2005). *Mikakati na Mbinu za Usimilishwaji katika Fasihi ya Watoto*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mwendwa, S. (2020). *Usimilisho wa Vielelezo katika Hadithi za Watoto na Namna Vinavyochangia katika Uwasilishaji Ujumbe*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mwendwa, S., Ngugi, P. M., na Ndungo, C. (2021). "Usimilishwaji wa Vielelezo katika Fasihi ya watoto. Mfano kutoka Wasifu wa Mwana Kupona (2008) na Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu (2015)". Katika, Shani O. Mchapange na Rhodah P. Kidami (Wah). *Kioo cha Lugha*. TATAKI. University of Dar es Salaam. Vol. 18. Kur 114-130.

Ndonye, L. (2017). *Rangi kama Mbinu ya Usimbaji Maana katika Diwani ya Rangi ya Anga*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nodelman, P. (1996). *The Pleasure of Children's Literature* (2nd ed.). NY: Longman.

Omuya, R. (2017). *Usimilishwaji wa Biblia kama Fasihi ya Watoto Hadithi Teule*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ruthiiri, M. K. (2012). *Tathmini ya Ufaafu wa Vitabu vya Kusoma kwa Madarasa ya 5 na 6 katika Shule za Msingi: Mifano ya Waandishi Wanne*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Schallert, D. L. (1980). "The Role of Illustrations in Reading Comprehension." In, *Theoretical Issues in Reading Comprehension*. Pp. 503-524.

Sever, S. (2012). *Children and Literature*. Izmir: Tudem.

Sheikh, A. A. na Nabhany, A.S. (1972). *Utendi wa Mwana Kupona: Utendi wa Ngamia na Paa*. Heinemann Educational Books.

Sohaimi, A. (2011). *Adaptation of Hikayat Hang Tuah in Children's Literature*. Malaysia: University of Utara.

10/2/2024 (Kwenye Mtandao).

Starrs, D. B. (2006). "A Queer New World: Adaptation Theory and the Zeugma of Fidelity in Derek Jarman's *The Tempest*." *The University of Melbourne*, Vol. Iv. Issue 1. <http://docs.google.com>. 10/3/2024

Tanaka, K. (1994). *Advertising Language: A Pragmatic Approach to Advertisements in Britain and Japan*. London: Routledge.

Tucker, N. (1984). *The Child and the Book*. Cambridge: Printed in Great Britain at the University Press.

TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: TUKI.

Tylor, J. (2017). *The Relationship Between Words and Images*. Retrieved <https://www.essaytyping.com/relationship-words-images/>. 02/02/2024.

Waffles, V. (2014). *On Character Design and Consistency*. Retrieved from <https://nilaffle.tumblr.com/post/77463153076/on-character-design-and-consistency>. 02/02/2024.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wiesner, D. (1991). *Tuesday*. New York: Houghton Mifflin Publisher.